**AGIZO>> Kuwepo kwa rejista ya migogoro ya ardhi inayoonesha ilivyotatuliwa.**

# Mtanda anyooshea kidole wenyeviti serikali za mitaa

**Na BALTAZAR MASHAKA,** *Ilemela*

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda amewataka watumishi wa Idara ya Ardhi, Manispaa ya Ilemela, kutatua kero na kuwahudumia wananchi kwa haki na kwa wakati.

Pia, amewanyooshea kidole baadhi ya wenyeviti wa serikali za mitaa kuwa wanaichonganisha serikali na wananchi kwa kuuza viwanja na kuzalisha migogoro ya ardhi, badala ya kufanya maendeleo.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki, alipozungumza na watumishi wa Manispaa ya Ilemela, kabla ya kukabidhi hati kwa wananchi watatu waliozitafuta kwa muda mrefu kutokana na kuzungushwa na wataalamu wa idara hiyo.

"Uhusiano baina ya wananchi na serikali ni muhimu, mwananchi ameufuatilia stakabadhi ya hati kwa miezi sita hapo Ardhi, wanatengeneza mazingira ya kufanya jambo liwe gumu, kuwakatisha tamaa, wapate rushwa. Hawa wanatugombanisha na wananchi," alisema.

Aliwataka watumishi wa umma kutojigeuza mangimeza, wafanye kazi ya kuendelea kujenga taswira nzuri ya CCM na serikali kwa wananchi kwa kutatua kero zao kwa wakati, badala ya kuwazungusha.

"Tumsaidie Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ana majukumu mengi. Wafanye kazi, tuwatendee watu haki haya mnayowafanyia mtafanyiwa pia, watendeeni wema mtalipwa kwa wema," alisema.

Kwa mujibu wa mkuu wa mkoa huyo, baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa, badala ya kufanya maendeleo wanasababisha migogoro kwa kuuza viwanja na kutengeneza miliki pandikizi.

Mtanda alisema kwa kufanya hivyo, wanaichonganisha serikali na wananchi, huku akiahidi uchaguzi utakapofika wataachwa kwa sababu wanashusha mvuto wa CCM na serikali yake kwa wananchi.

Aidha, aliagiza kuwepo na rejista ya migogoro ya ardhi jinsi ilivyotatuliwa.

"Wenyeviti wa mitaa wanaouza viwanja na kusababisha migogoro, hawasomi mapato na matumizi kwa wananchi, hao ni bora waondolewe mapema," alisema.

Kwa upande wa wananchi waliokuwa wakizungushwa kupewa hati zao, licha ya kulipa wakiambatanisha na nyaraka muhimu, Immaculata Tenga na Anna Andrew (wajane) na Kimenye Gisimba walimshukuru Mtanda kwa kutatua kero yao ndani ya siku moja.

"Tangu mwaka 2015 nimefuatilia hati bila mafanikio na kila nikija Ardhi wananiambia njoo kesho, njoo kesho, kwa kweli Rais Dk. Samia amemleta mkuu wa mkoa anayefahamu kutatua kero za wananchi kwa kuwa nilifuatilia hati kwa muda mrefu. Mwenyezi Mungu akubariki uendelee kufanya kazi yako, kama ulivyofanya kwetu," alisema.

Anna Andrew alisema amefuatilia hati yake halmashauri kwa miaka miwili, akisafiri kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, lakini ameipata ndani ya siku moja.

"Nilivyomsikiliza mkuu wa mkoa huyu (Mtanda) natamani kurudi tena Mwanza, nilihama sababu ya kuchukizwa na kuumizwa na vitu vingi, sasa natamani kurudi, ingekuwa ni kupiga kura ningepiga aendelee kubakia hapa, lakini sina uwezo huo," alisema mjane huyo.

Naye, Gisimba ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Ualimu Murutunguru, alisema licha ya kulipia gharama za hati na kuwasilisha nyaraka, hakupewa kwa miezi sita, hivyo alimpongeza Mtanda kwa kuwawezesha kupata hati zao ndani ya siku moja.

Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala alisema wamepokea ushauri wa kuonesha njia watumishi waliopewa dhamana ya kuwahudumia wananchi hususan viongozi wanaowasimamia watumishi wa chini yao.

## Wananchi wahamasishwa kutumia mfumo e-Mrejesho

**Na MWANDISHI WETU**

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (e-GA), imewasihi wananchi kuendelea kutumia mfumo wa e-Mrejesho kuwasiliana na serikali kwa kutoa hoja, maoni na ushauri zifanyiwe kazi.

Meneja Mawasilino wa e-GA, Subira Kaswaga alitoa wito huo, Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki, alipozungumza na waandishi wa habari akiwa banda la eGA, katika maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) maarufu Sabasaba. Maonesho hayo yalihitimishwa juzi.

Subira alieleza mfumo huo umejengwa kama daraja linalowawezesha mwananchi kuwasiliana na serikali na kusikilizwa hoja zao na kufanyiwa kazi.

Aliwataka wananchi kuitumia e-GA ikiwa jukwaa la kuwasiliana na serikali.

Mbali na hilo, Subira alieleza hivi sasa mamlaka na taasisi za serikali zinabadilishana taarifa na kusoma kidijitali, hivyo mamlaka hiyo inahamasisha taasisi zote za umma kujiunga na eGA kuwa pamoja kidijitali.

"Kwa hiyo sisi tumetengeneza mfumo huo na tayari tumeshaunganisha mifumo mbalimbali na hivi sasa tunachokifanya ni kuzihamasisha taasisi za umma zijiunge na mfumo huo zibadilishane taarifa," alisema.

Alisema hadi hivi sasa, taasisi zilizounganishwa na mfumo huu ni 141 na mifumo 148 imeshaunganishwa, kati ya mifumo hiyo, 109 inasomana na kubadilishana taarifa.

Miongoni mwa taasisi hizo ni Mahakama, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na Jeshi la Polisi.

## PONGEZI



**DIWANI wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule (kushoto), akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Majestic Kimpili, baada ya kufunga kikao cha Baraza la UVCCM la kata hiyo, Dar es Salaam, jana. Katikati ni Katibu wa CCM Kata ya Kivukoni, Saidi Mwanga. (Na Mpigapicha Wetu).**

# Kampuni ya uwakili yawasilisha maombi kulipwa milioni 500/-

**Na MWANDISHI WETU**

MAOMBI ya Kampuni ya Mawakili ya Dar es Salaam Kings Law Chamber ya kudai zaidi ya sh. milioni 500 yanatarajiwa kutajwa Julai 24, mwaka huu, katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Kampuni hiyo inadai fedha hizo kutoka Benki ya NCBA Tanzania Limited, zikiwa malipo ya kitaalamu kwa kuendesha kesi ya mgogoro wa kibiashara.

Shauri hilo linatarajiwa kutajwa mbele ya Msajili Joyce Minde.

Inadaiwa fedha hizo zinajumuisha dola za Marekani 168,573.33 ambazo ni asilimia tatu ya jumla ya dola za Marekani 4,265,625 zenye utata katika kesi ya kibiashara namba 12 ya 2023, ambayo kampuni hiyo ilitoa huduma za kitaalamu.

Aidha, dola 25,250 ni za kuhudhuria kikao cha kukadiria malipo.

Maombi hayo yaliwasilishwa mahakamani hapo, yakiungwa mkono na hati ya kiapo cha Wakili Emanuel Makene ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo.

Katika kiapo hicho, Wakili Makene alidai waombaji walipewa kandarasi na Benki ya NCBA (mlalamikiwa), chini ya Makubaliano ya Ujira ya Oktoba 29, mwaka 2021 yenye lengo la kutoa huduma za uwakili kwa kuzingatia malipo ya asilimia tatu ya suala hilo.

Inadaiwa mkataba uliandaliwa na mlalamikiwa alitia saini.

Alidai waombaji hawakumwomba mjibu maombi kwa kazi yoyote na ilikuwa ni uamuzi wa upande mmoja wa mlalamikiwa kuwapa mkataba waombaji, baada ya mawakili wengine kushindwa katika kesi kama hiyo.

Aliendelea kudai mlalamikiwa alimlazimisha mwombaji kulipia fidia ya bima ya kitaalamu ambayo ililipwa, kwa upande wa mlalamikiwa yenye thamani ya kuanzia sh. milioni 800 hadi sh. bilioni moja.

Wakili huyo alidai bima hiyo, itamlipa mlalamikiwa hadi sh. milioni 800 endapo mlalamikiwa atapoteza kesi mahakamani kutokana na makosa ya kitaaluma yaliyofanywa na waombaji.

"Waombaji walilipa shilingi 8,260,000 kwa mwaka mmoja wa Mkataba wa Malipo kwa kampuni ya bima, iitwayo Britam Insurance Tanzania Limited. Waombaji wanalazimika kulipa Britam Insurance Tanzania Limited shilingi milioni 8,260,000 kila mwaka katika kipindi cha uhai wa Mkataba wa Ujira," alidai.

Alidai walimwakilisha mlalamikiwa katika kesi ngumu, aliyowashitaki wakopaji na alikuwa anadai zaidi ya dola za Marekani 4,265,625.

Wakili huyo alidai mgogoro huo ulitokea Machi 7, mwaka huu, mlalamikiwa alipokataa kuwalipa waombaji dola za Marekani 168,573.33, ambayo ni asilimia tatu ya dola 4,265,625 zilizobishaniwa, chini ya Mkataba wa Oktoba 29, mwaka 2021.

"Kesi pia ilikuwa ngumu zaidi kwa sababu mlalamikiwa alitoa mkopo kwa wakopaji wa thamani ya dola za Kimarekani 3,250,000 bila kuweka mali yoyote kama dhamana," alidai wakili huyo kupitia hati ya kiapo.

Aliendelea kudai hauri kuu lilikuwa gumu kutokana na kwamba, Kampuni ya Bima (UAP Insurance Tanzania Limited) iliyokuwa sehemu ya Mkataba wa Mkopo kati ya mlalamikiwa na wakopaji; ilishitakiwa na mlalamikiwa katika kesi ya kibiashara namba 131 ya mwaka 2018, bila kujiunga na wakopaji na mlalamikiwa alishindwa kesi hiyo.

Wakili Makene alidai mlalamikiwa aliwaagiza waombaji kusajili kesi mahakamani kabla ya Desemba, mwaka 2022 au mara moja na siyo zaidi ya Februari, mwaka jana. Mlalamikiwa hakuwa katika nafasi ya kuwalipa waombaji ada za awali za uwakili, wala ada za mahakama kwa mujibu wa mkataba wa malipo.

**MAOMBI**

**HATI YA KIAPO**

Katika kiapo hicho, Wakili Makene alidai waombaji walipewa kandarasi na Benki ya NCBA (mlalamikiwa), chini ya Makubaliano ya Ujira ya Oktoba 29, mwaka 2021 yenye lengo la kutoa huduma za uwakili...

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

SIMBA MTOTO TRANSPORT inatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SCANIA yenye namba za usajili T 796 DKT Chassis Na.3876204, Engine Na. 8263987 Taarifa hii imetolewa katika kituo cha Polisi TANGA na kupewa Kumbu Namba PHQ/TAN/TAN/7020/2024 Yeyote atakayeipata aipeleke katika kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu naye.

15033